


Msaada Wa Matibabu kwa Wakimbizi

MWONGOZO KUHUSU MANUFAA

Kiswahili



UTANGULIZI

Kamati ya Marekani ya Wakimbizi na Wahamiaji (USCRI) imekuwa ikishughulikia mahitaji na kutoa utetezi kwa niaba ya wakimbizi na wahamiaji tangu 1911. USCRI inasimamia mpango wa Msaada wa Matibabu kwa Wakimbizi (RMA) kwa wageni ambao hawajaidhinishwa kupata misaada ya matibabu katika mipango ya Medicaid kwenye majimbo yao. RMA ina manufaa ya matibabu ya kawaida, matibabu ya meno, matibabu ya macho na huduma za famasia kama ya Medicaid. Mwongozo huu wa Manufaa unakufahamisha jinsi ya kupata manufaa ya RMA.

Manufaa ya RMA hushughulikiwa na Point Comfort Underwriters, Inc. (PCU).



MSAADA WA MATIBABU KWA WAKIMBIZI

Je, ninastahiki kupokea manufaa ya RMA?

Ili kujua ikiwa unastahiki kupokea RMA ni lazima ukamilishe fomu ya ombi la RMA. Meneja wako wa shirika la makazi katika eneo lako anaweza kukusaidia kutuma ombi. Kwa ujumla, utaruhusiwa ikiwa unatimiza masharti yafuatayo:

1. Ikiwa hali yako ya uhamiaji ni mkimbizi au hali nyingine inayofaa.
2. Unatimiza masharti ya kutambuliwa kuwa mhamiaji.
3. Unatimiza kiwango cha mapato.
4. Huruhusiwi kupokea msaada wa Medicaid, Bima ya Afya ya Watoto au bima nyingine ya afya ya binafsi au ya umma.

Ninaweza kusaidiwa na RMA kwa muda upi?

Manufaa yako ya RMA hukatizwa moja kwa moja miezi 8 baada ya kufika Marekani. Ongea na meneja wa kesi yako kwenye shirika la makazi lililo katika eneo lako kwa maelezo zaidi kuhusu hali yako.

Kumbuka kuwa ukihama kwenye jimbo la Maine, ni lazima uarifu shirika la makazi lililo katika eneo lako na hutaruhusiwa kupokea manufaa ya RMA ya Maine.

KITAMBULISHO CHA RMA


Kitambulisho cha RMA ni nini?

Watu wote wanaoandikishwa kwenye mpango wa RMA hupokea kadi binafsi za Kitambulisho cha RMA. Unaweza kupata kitambulisho chako kwenye shirika la makazi lililo katika eneo lako. Pia unaweza kuomba kadi ya Kitambulisho cha RMA kutoka PCU. Wapigie PCU simu au tuma barua pepe kwa service@pointcomfort.com.

Kadi yako ya Kitambulisho ya RMA ina jina lako, nambari yako ya utambulisho na maelezo mengine muhimu kuhusu manufaa ya RMA. **Ni lazima uonyeshe kadi yako ya Kitambulisho cha RMA kila wakati unapokea huduma.** Ikiwa zaidi ya mtu mmoja wa familia yako ameandikishwa katika RMA, kadi tofauti ya kitambulisho itatolewa kwa kila mwanafamilia. Ni mtu mmoja tu ambaye ametajwa kwenye kadi ya kitambulisho ndiye anaweza kutumia kadi. **Usimwazime au kumpa mtu mwingine kadi yako ya kitambulisho.**

Nitatumiaje kadi yangu ya kitambulisho cha RMA?

Unafaa kuwa na kadi yako ya kitambulisho cha RMA kila wakati. Onyesha kitambulisho chako kwa daktari, hospitali, daktari wa meno au famasia unapohitaji huduma. Watoaji huduma wako watatumia kadi hii ya kitambulisho ili kuthibitisha kuwa unafaa kupokea manufaa ya RMA na kupata habari muhimu kuhusu anayefaa kulipia huduma unazopokea. **Kukosa kuwasilisha kadi yako ya kitambulisho kwa watoaji huduma kutasababisha kuchelewa kwa malipo ya madai na unaweza kupoteza manufaa.**



Nini kitafanyika nikipoteza kadi yangu ya kitambulisho cha RMA?

Unaweza kupata kadi mpya ya kitambulisho kutoka PCU. Wasiliana na PCU kwenye service@pointcomfort.com. Huenda ukahitajika kutoa maelezo ya kibinafsi ili PCU iweze kuthibitisha utambulisho wako kabla ya kupewa kitambulisho kingine.

Ikiwa maelezo binafsi kama anwani ya nyumbani kwako, nambari ya simu au anwani ya barua pepe yatabadilika, hakikisha umeifahamisha PCU kwenye service@pointcomfort.com. Hakikisha kuwa PCU ina anwani yako ya barua pepe unayoitumia kila wakati.

HUDUMA ZA AFYA

Ninaweza kutembelea vituo gani vya huduma za afya?

Unaweza kuhudumiwa na mtoa huduma yeyote anayekubali malipo kulingana na viwango vya malipo vilivyoidhinishwa na mpango wa RMA. Unaweza kupata orodha ya watoa huduma ambao wamekubali viwango hivi kwenye rma.pointcomfort.com, au kupigia PCU simu ili kusaidiwa. Ikiwa unataka kutumia mtoa huduma ambaye hayuko kwenye orodha hii, unafofaa kufanya mambo yafuatayo:

1. Pata jina kamili, anwani na nambari ya simu ya mtoa huduma unayetaka kumtumia.
2. Wapatie PCU maelezo haya

PCU itawasiliana na mtoa huduma na kujaribu kupata makubaliano ya kutoa huduma kwa viwango vya malipo vilivyoidhinishwa. PCU itakwambia matokeo ya majadiliano haya.

Kumbuka kuwa unafaa kuenda kwenye Chumba cha Dharura kilicho karibu zaidi wakati wa dharura.

Ni huduma zipi za matibabu zinalipiwa na bima?

RMA hulipia huduma nyingi za afya wakati ambapo zinahitajika kiafya na kulingana na masharti fulani: Zifuatazo ni baadhi ya huduma zinazolipiwa:

ADA ZA HOSPITALI

- Chumba cha kila siku, huduma za malazi na uuguzi kwenye wadi au chumba kilicho cha binafsi kiasi.
- Chumba cha kila siku, huduma za malazi na uuguzi kwenye Chumba cha Wagonjwa Mahututi
- Matumizi ya vyumba vya upasuaji, matibabu na vya wanaopata nafuu
- Bendeji, nyuzi za kushona na bidhaa nyingine za kawaida wanazopewa wagonjwa waliolazwa
- Matibabu katika Chumba cha Dharura (ni lazima yawe ya dharura)
- Dawa anazoandikiwa mgonjwa aliyelazwa
- Huduma za radiolojia, maabara na upigaji picha za 'Ultrasound'.
- Matibabu ya kimwili, matibabu ya kikazi na matibabu ya kuzungumza unapokuwa umelazwa
- Huduma za wataalamu, wakiwemo madaktari

HOSPITALI YA KUTIBIWA BILA KULAZWA/ HUDUMA ZA UPASUAJI AMBAKO MGONJWA HALAZWI

- Huduma za wataalamu, wakiwemo madaktari
- Bendeji, nyuzi za kushona na bidhaa za kawaida wanazopewa wagonjwa wasiolazwa

KUTEMBELEA DAKTARI NA KLINIKA

- Madaktari na wataalamu
- Matibabu ya kimwili, matibabu ya kikazi na matibabu ya kuzungumza
- Wataalamu wa Afya ya Kiakili/Kitabia walio na leseni
- Huduma za radiolojia, maabara na upigaji picha za 'Ultrasound'.
- Huduma za maungo na neva

HUDUMA NYINGINE ZINAZOLIFIWA

- Usafiri wa dharura wa ambulensi mahali ulipo
- Vifaa vya matibabu vinavyodumu
- Huduma za afya nyumbani
- Utunzaji wa wagonjwa wanaogua kwa muda mrefu
- Matibabu ya kutumia miale
- Tibakemikali
- Hemodayalasisi
- Oksijeni na gesi nyingine na matumizi yake
- Dawa za kutia ganzi na matumizi yake
- Uchunguzi mmoja wa kuona na miwani moja
- Huduma za kusikia ikiwemo kupewa dawa, kuweka au kubadilisha visaidizi vya kusikia
- Huduma za ukalimani ikiwa zinatolewa na daktari anayetibu

Ni huduma zipi za matibabu ambazo hazilipiwi na bima?

- Gharama za mimba na mtoto aliyezaliwa
- Vitu vya matumizi ya binafsi
- Mashauriano kupitia kwa simu au kukosa kufika kwa miadi iliyopangwa
- Mabadiliko yoyote ya mwili yanayolenga kuboresha hali ya kisaikolojia, kiakili na kimawazo
- Mipango ya michezo, iwe imependekezwa na daktari au la
- Utaratibu wowote wa kuboresha sura au urembo
- Matibabu ya kutoshika mimba, kutozalisha au matatizo ya kingono
- Huduma au vifaa vinavyotumika kwa ajili ya kufanya uchunguzi, majaribio au kutafti.
- Upasuaji wa macho ili kurekebisha kuona kwa karibu tu, kuona kwa mbali tu au tatizo linalozuia fokasi
- Utaratibu wa kumfunza mgonjwa kurekebisha shughuli za mwili, kufurahia, kulala au matibabu ya muziki.

DAWA UNAZOANDIKIWA

Ninaweza kutumia famasia ipi?

Dawa unazoandikiwa hutolewa kupitia kwa Mtandao wa famasia wa MagellanRx Management. Mtandao huu unajumuisha maduka yote makuu, kama Walmart na CVS, na matawi na maduka mengi katika eneo lako. **Ni lazima uonyeshe kadi yako ya kitambulisho kwa mfamasia kila wakati unapohitaji kupata dawa ulizoandikiwa.** Mfamasia atathibitisha ikiwa dawa ziko kwenye mtandao na iwapo unastahiki kupokea huduma za bima za dawa unazoandikiwa.

Ni dawa gani unazoandikiwa ambazo hazilipiwi na bima?

- Dawa asilia wakati dawa za kawaida kama hizo zinapatikana
 - Dawa yoyote inayohusiana na matibabu yasiyo katika mpango huu
 - Dawa unazoweza kununua bila kuandikiwa na daktari
- Idadi ya juu zaidi ya siku za kutumia dawa ni siku 30

- Huduma au vifaa vinavyotolewa na jamaa yako au mtu yeyote anayeishi nawe
- Huduma au vifaa vinavyotolewa bila malipo
- Gharama za usafiri na makazi
- Matibabu ya kusaidia ukuaji wa nywele, yawe yamependekezwa na daktari au la.
- Matibabu ya kuzuia kupoteza nywele
- Matibabu ya matatizo ya kulala
- Huduma yoyote au kifaa ambacho si Lazima Kiafya
- Kutolewa kwa vifaa ambapo manufaa au malipo yanatolewa kupitia sera au mikataba mingine

(Baadhi ya hali za kipekee hazitumiki kwa watu walio na umri wa chini ya miaka 21. Wasiliana na PCU kwa maelezo zaidi.)

MATIBABU YA MENO

Naweza kuhudumiwa na tabibu yupi wa meno?

Unaweza kuhudumiwa na daktari yeyote wa meno aliye kwenye Mtandao wa DenteMax. Unaweza kupata orodha ya madaktari wa DenteMax kwenye www.dentemax.com/findadentist, au kupigia PCU simu ili kupata usaidizi. Madaktari wa DenteMax pekee ndio wameidhinishwa kutoa huduma za meno za RMA. **Ni lazima uonyeshe kadi yako ya kitambulisho cha RMA kwa Tabibu wa Meno kila unapohitaji huduma za afya za meno.**

Ni huduma zipi za matibabu ya meno ambazo zinalipiwa na bima?

- Matibabu ya dharura ya meno yanayohitajika ili kupunguza uchungu au kuzuia maambukizi
- Matibabu ya dharura ya meno yanayotokana na ajali

Uidhinishaji wa awali hauhitajiki kwa matibabu ya dharura.

Ni huduma zipi za matibabu ya meno ambazo hazilipiwi na bima?

Huduma zilizo rodheshwa tu ndizo hulipiwa.

UIDHINISHAJI WA AWALI

Ni huduma zipi ambazo ni lazima ziidhinishwe kabla ya kutibiwa?

Huduma nyingi zinazoshughulikiwa ni lazima ziidhinishwe kabla ya kutibiwa. Hiyo inamaanisha kuwa ni lazima upokee idhini ya PCU kabla ya kutibiwa. Huduma zifuatazo ndizo uidhinishwa kabla ya kutibiwa:

- Utunzaji wa mgonjwa aliyelazwa
- Upasuaji wa aina yoyote
- Utunzaji kwenye kituo cha wanaogua kwa muda mrefu
- Utunzaji wa wagonjwa wanaogua kwa muda mrefu
- Huduma za kiafya nyumbani
- Utunzaji wa maungo na neva
- Matibabu ya kimwili
- Matibabu ya kikazi
- Matibabu ya mazungumzo
- Kupimwa kwa mizio
- Vifaa vya matibabu vinavyodumu
- Utunzaji wa kiafya ya kiakili/kitabia
- Miguu au mikono bandia
- Viungo bandia
- Tomografia za Kompyuta (Skani za CAT)
- Utaratibu wa Kupiga Picha za Viungo kwa Miale ya Sumaku (MRI)
- Kupandikizwa kwa viungo/tishu za binadamu

Nitapokeaje Uidhinishaji kabla ya kutibiwa?

Punde tu unapojua kuwa unaenda kupokea huduma inayohitaji uidhinishaji kabla ya kutibiwa, mtoa huduma wako anafaa kuwasiliana na PCU kwenye RMAClinical@pointcomfort.com au kwa simu. Utahitaji kutaja jina lako, nambari ya kitambulisho, jina la mtoa huduma unayetaka akuhudumie na maelezo yake ya anwani, na maelezo kuhusu tiba iliyopangwa. Mara nyingi, PCU hutoa idhini moja kwa moja; lakini wakati mwingine uidhinishaji wa awali unaweza kuchukua hadi saa 48 kukamilika. Hiyo ndiyo sababu inafanywa iwe muhimu kuwasiliana na PCU punde tu unapojua utaenda kupokea matibabu.

Uidhinishaji wa awali hauhitajiki kwa matibabu ya dharura; lakini ni lazima utafute idhini ya awali haraka iwezekanavyo.

Wakati mwingi, mtoa huduma wako atakuanzishia mchakato wa kutafuta idhini ya awali. Atahitaji maelezo yaliyomo kwenye kadi yako ya kitambulisho cha RMA. Watoa huduma wanaweza kutuma maombi yao ya idhini ya awali kwa PCU kwenye pcf.pointcomfort.com.

Unafaa kuonyesha kadi yako ya kitambulisho cha RMA kila unapohitaji huduma.

Nini kitafanyika nikipokea tiba bila uidhinishaji wa awali?

Ikiwa una matibabu yanayohitaji idhini ya awali lakini ukose kutafuta idhini kabla ya kutibiwa, inamaanisha utalipa gharama za tiba hiyo.

RUFAA

Nini kitafanyika ikiwa sikubaliani na uamuzi wa dai au idhini ya awali?

Unafaa kuanza mchakato wa kuomba rufaa kwa kufuata hatua hizi:

1. Kupiga simu au kuandikia PCU barua na utoe maelezo kamili kuhusu rufaa yako, ndani ya siku 30 tangu siku ulipopokea uamuzi kuhusu dai au Idhini ya awali. Ni lazima ujumlishe majina na maelezo ya anwani za watoa huduma wote wanaohusika katika utunzaji wako.
2. Ndani ya siku 10 za kazi, PCU itakujibu kwa kukiri kuipokea na kukupa wakati uliokadiriwa kukamilisha uchunguzi unaohitajika.
3. Ndani ya siku 30, PCU itakupatia jibu lilioandikwa lenye maelezo kuhusu hali ya rufaa yako.

FARAGHA

Kila wakati unapopokea huduma ya afya, daktari wako huandika kilichofanyika na kuweka maelezo hayo kwenye faili yako. Faili hii inahifadhiwa kwa faragha. Daktari wako anaweza kuwapatia wengine faili yako ukikubali tu.

PCU inatakiwa kuhifadhi kwa faragha maelezo kuhusu afya yako. PCU inaweza kuwapatia washirika wengine maelezo yako ukikubali tu.

Una haki ya kupata nakala za rekodi zako za matibabu kutoka kwa watoa huduma wako na PCU Pia unaweza kuomba mabadiliko yafanywe kwenye rekodi zako ikiwa unajua kuna jambo lisilo sahihi. Huenda ukahitajika kuwalipa watoa huduma wako au PCU ada kwa gharama za kupiga chapa.

ORODHA YA HUDUMA ZAKO ZA RMA

Maswali kuhusu ustahiki au bima:

Service@pointcomfort.com

1-844-210-2010

Maswali kuhusu mitandao ya watoa huduma:

Matibabu ya kawaida na ya Meno:

Providers@pointcomfort.com

1-844-210-2010

rma.pointcomfort.com

Dawa Unazoandikiwa:

RxNetworksDept@magellanhealth.com

1-800-424-0472

Uidhinishaji wa awali:

RMAClinical@pointcomfort.com

1-844-210-2010

rma.pointcomfort.com

Hali ya Dai:

Service@pointcomfort.com

1-844-210-2010

claims.pointcomfort.com

Rufaa:

Claims@pointcomfort.com

1-844-210-2010